

HAKIRASILIMALI YAIPONGEZA WIZARA YA MADINI KWA UWAZI

DODOMA

28 MEI 2019

HakiRasilimali, mtandao wa asasi za kiraia unaofanya uchechemuzi katika sekta ya madini, mafuta na gesi, jana tarehe 27 Mei 2019 imeipongeza Wizara ya Madini kwa kuonesha uwazi katika fedha zilizopatikana kutokana na Mauzo ya Madini hususani madini ya almasi tangu kuanzishwa kwa masoko ya madini takribani 14 katika mikoa mbalimbali nchini baada ya mkutano mkuu wa wadau sekta ya madini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli. Januari 22 mwaka 2019. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Wizara ya Madini, kiasi cha Shilingi milioni 238 kilipatikana kama kodi ya Serikali baada ya mchimbaji mdogo kuuza almasi yake kwa kiasi cha Shilingi Bilioni 3 kwenye soko la madini la Shinyanga. Tukio hili lilishuhudiwa na Naibu Waziri wa Madini Mh. Stanslaus Nyongo.

“Ni jambo la kihistoria, kwa muda mfupi kwa kuanzishwa kwa masoko haya ufanisi wake kuonekana hususani pale jiwe la almasi kubwa kiasi hichi kuuzwa kwenye soko la ndani. Ni vizuri, kupanua wigo wa uwazi katika sekta ya madini ili kuhusisha madini ya aina nydingine kama vile Tanzanite, dhahabu, Nickel na cobalt,” alisema Bwana Semkae Kilonzo, Makamu Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi ya HakiRasilimali.

Halikadhalika, ili kuboresha mfumo mzima wa uwazi katika sekta ya Uziduaji, HakiRasilimali imeiomba serikali kuupatia rasilimali fedha za kutosha mpango wa uwazi na uwajibikaji katika sekta ya madini, mafuta na gesi (TEITI) ili kuongeza ufanisi wa taasisi husika. Sambamba na hayo, HakiRasilimali inaishauri Wizara ya Madini kuiwezesha TEITI kukabiliana na upungufu wa rasilimali watu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya taasisi.

Bi. Racheal Chagonja, Mratibu wa HakiRasilimali, alisema: “*Ili taasisi iwe na ufanisi zaidi ni vizuri kuimarishe muundo na mfumo wa mamlaka, utendaji, maamuzi na utashi wa kisisasa kwa kukifanya chombo hiki kuwa huru zaidi. Hata hivyo tunaipongeza sana Serikali kwa dhamira njema ya kuanzisha na kulea mpango huu kabambe wenye tija kwa nchi yetu, tuna imani kubwa na nia ya Serikali na wadau wengine wa maendeleo katika kuifanya TEITI kuwa imara zaidi na yenyе kuwajibika ipasavyo.*”

Registration No. 133413

Board of Directors: Chairperson: - Donald Kasongi – Governance Links • Vice Chairperson: - Semkae Kilonzo-Policy Forum • Members • Stephan Msechu-Tanganyika Law Society: - Amani Mustapha Mhinda – HakiMadini • Moses Kulaba – Governance and Economic Policy Centre (GEPC) • Secretary: - Racheal Chagonja

Pia, HakiRasilimali inaishauri serikali kupitia tovuti ya wizara ya madini kuweka wazi mikataba ya madini kwa kuzingatia kwamba, msingi mkuu wa kuanzishwa TEITI ni kwa ajili ya kukuza na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini.

Kwa taarifa zaidi au kuomba mahojiano, wasiliana na HakiRasilimali info@hakirasilimali.or.tz / +255 745 655 655